



MAGEUZI MAKUBWA

# Miaka minne ya Rais Samia madarakani: Mzumbe wajivunia mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk Samia Suluhu Hassan (kulia) akitunikiwa Shahada ya Udaktari wa heshima katika uongozi na Mkuu wa Chuo cha Mzumbe, Dk Ali Mohammed Shein.

Chuo Kikuu Mzumbe ni taasisi ya umma ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Chuo Kikuu Mzumbe Na. 21 ya mwaka 2001. Sheria hiyo ilifutwa na Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005 ambayo inasimamia masuala yote yanayohusu elimu ya vyuo Kikuu nchini Tanzania. Kwa sasa, Chuo kinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Hati Idhini ya Chuo Kikuu Mzumbe, 2007 iliyotolewa chini ya Kifungu Na. 25 cha Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005.

Chuo kimeendelea kukua kwa kasi ambapo hadi sasa kina jumla ya wanafunzi 16,462 kutoka Kampasi kuu -Morogoro, ndaki ya Mbeya pamoja na ndaki ya Dar es Salaam (kampasi kuu 11,284, Mbeya 3,385 na Dar es Salaam 1793). Kati ya hao, wanafunzi 8356 sawa na asilimia 51 ni wanaume, na wanafunzi 8,106 sawa na asilimia 49 ni wanawake.

Chuo kina matawi matatu, yaani, Kampasi Kuu iliyopo Morogoro, Kampasi ya Dar es Salaam, kampasi ya Mbeya na kinaendelea na ujenzi wa kampasi mpya ya Tanga inayofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation-HEET).

Majukumu makubwa ya Chuo Kikuu Mzumbe ni kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya utafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kutoa huduma kwa jamii. Chuo Kikuu Mzumbe kinaendesha programu 77 za masomo katika fani mbalimbali na kwa ngazi tofauti zikiwemo Astashahada nane, Stashahada saba, Shahada za Kwanza 30, Shahada za Umahiri 26 na Shahada za Uzamivu ("PhD") katika maeneo yote ya ubobezi yanayotolewa Chuo Kikuu Mzumbe.

Chuo Kikuu Mzumbe kimejijengea umahiri na ubobevu kwa miaka mingi katika fani za Utawala wa Umma, Menejimenti ya Rasilimali Watu, Serikali za Mitaa, Mifumo ya Afya na Mazingira, Ufuatiliaji na Tathmini Katika Afya.

Chuo Kikuu Mzumbe pia kimebobea katika Uongozi wa Biashara, Ujasiriamali na Ubunifu; Uhasibu na Fedha, Ununuzi na Ugavi, Uchumi ikiwa ni pamoja na Mipango na Sera, Mipango na Menejimenti ya Miradi na Maendeleo ya Watu, Sheria, Elimu (Hisabati na Lugha, Biashara na Uhasibu), Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Menejimenti ya Mifumo, Menejimenti ya Habari na Mawasiliano), Sera za Umma, Menejimenti ya Uhandisi wa Viwanda na Menejimenti ya Uzalishaji na Usimamizi.

Chuo Kikuu Mzumbe kimeendelea kuwa taasisi bora ya elimu ya juu nchini Tanzania, kikijivunia historia yake ndefu ya kutoa wataalamu na viongozi mahiri kwenye nyanja mbalimbali. Kati ya viongozi wengi waliosoma Chuo Kikuu Mzumbe kwenye masuala ya uongozi na kufanikiwa kushika nafasi za juu katika uongozi ni pamoja na Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dk Samia Suluhu Hassan.

Jumuiya ya Chuo Kikuu Mzumbe inayo kila sababu ya kuona fahari na kujivunia mafanikio lukuki yaliyopatikana katika kipindi cha utawala wake kwani umahiri aliouonesha kama kiongozi mkuu na uzalendo wake kwa nchi ni uthibitisho wa kutosha kudhihirisha kuwa yeye ni mmoja wa wahitimu bora wa Utawala wa Umma waliosoma katika Chuo hiki.

Katika kipindi kifupi cha uongozi wake wa miaka minne, Dk Samia Suluhu Hassan ameliwezesha taifa la Tanzania kupiga hatua kubwa kwenye nyanja zote za maendeleo nchini ikiwemo uboreshwaji wa miundombinu, huduma za jamii na uchumi lakini kubwa zaidi ambalo makala hii itaangazia ni mapinduzi makubwa kwenye sekta ya elimu na kwa namna ya kipekee Chuo Kikuu Mzumbe kilivyonufaika na Uongozi wake ambao umekuwa chachu ya mabadiliko makubwa, hususan kwenye ubora wa elimu ya juu, utafiti, ushirikiano wa kimataifa, na kuboresha mazingira ya kujifunza.

**Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET)**

Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ni juhudi za Serikali ya Tanzania, chini ya Rais Samia Suluhu Hassan za kuboresha sekta ya elimu ya juu ili kuchangia katika mageuzi ya kiuchumi ya nchini. Mradi huu unatekelezwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia na umelenga kuboresha miundombinu ya elimu ya juu, kuongeza fursa za udahili, na kuhamasisha ubunifu miongoni mwa wanafunzi.

Chuo Kikuu Mzumbe ni moja kati ya Taasisi za Elimu ya Juu ambazo zimenufaika na mradi huo kwa kupatiwa kiasi cha Dola milioni 21 za kimarekani (takribani Sh 50 bilioni) kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya kujifunza na kufundishia pamoja na kuanzisha kampasi mpya mkoani Tanga.

Tangu kuanza kwa mradi huo mwaka 2021 Chuo Kikuu Mzumbe kimepiga hatua kwenye utekelezaji wa mradi huo ambapo kwa sasa kinaendelea na ujenzi wa majengo ya kisasa ya taaluma na kituo cha TEHAMA katika kampasi kuu na ujenzi wa kampasi ya Tanga.

Aidha ili kuendana na malengo ya mradi wa HEET ya kuzalisha wahitimu wenye ujuzi unaohitajika sokoni ambao watakuwa na uwezo wa kuchagiza uchumi na kuchangia maendeleo endelevu ya taifa, Chuo kimefanya mapitio ya mitaala kwa programu za shahada za awali pamoja na kuanzisha programu mpya.

**10,454**

**Wanafunzi walionufaika na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Chuo Kikuu Mzumbe mwaka 2024/25.**

Jumla ya programu 10 ziko katika hatua za mapitio na programu 11 mpya ziko katika hatua mbalimbali za mchakato wa kuanzishwa. Hadi sasa jumla ya programu 20 zimewasilishwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa ajili ya maombi ya kupatiwa ithibati.

Kadhalika kwa upande wa programu za shahada za umahiri Chuo kimeendelea kuchukua hatua za kimkakati kuboresha mitaala yake pamoja na kuanzisha programu za kimkakati. Baadhi ya programu zinazotarajiwa kuanzishwa ni pamoja na Master of Implementation Science (MIS), Master of Digital Finance, Master of Law in ICT Law, Master of Development Monitoring & Evaluation (MDME), na Master of Arts in Kiswahili (MAK).

Kupitia mradi wa HEET Chuo pia kimeanza usanifu wa miundombinu ya maktaba ya kidijitali na mtandao (digital and virtual library infrastructure). Aidha kimeweza kutengeneza studio (multimedia) yenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya kusaidia ufundishaji wa masomo kwa njia ya mtandao (Blended Learning) na kimeweza kununua samani za kituo cha msaada kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, vikiwemo kompyuta, vifaa vya teknolojia saidizi (Assistive and adaptive technologies) na vitabu vya maktaba n.k.

Thamani ya jumla ya vifaa vyote hivyo ni takribani Sh 2.4 bilioni. Inategemewa kwamba kukamilika kwa miundombinu itakayojengwa kupitia mradi wa HEET, idadi ya wanafunzi itaongezeka kutoka 16,462 waliopo sasa hadi takribani wanafunzi 17,000 mwaka 2026/27.

Benki ya Dunia imeonyesha kuridhishwa na hatua za utekelezaji wa mradi huu kwa Chuo Kikuu Mzumbe kwani hivi karibuni ujumbe ulioambatana na ujumbe kutoka wizara ya Elimu na Sayansi na ulitembelea na kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo ambapo waliridhika na kuipongeza Menejimenti ya Chuo kwa kusimamia vyema mradi huo.

**Mikopo ya elimu ya juu**

Wanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe wamekuwa wanufaika wakubwa wa mikopo ya elimu ya juu ambapo idadi yao imeendelea kuongezeka kutoka 7,434 mwaka 2022 hadi kufikia 10,454 mwaka 2025.

Kiasi cha zaidi ya Sh 32.13 bilioni kilitolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kulipia gharama za malazi, chakula, masomo n.k.

Ongezeko hilo linafanya jumla ya wanafunzi 3,109 kunufaika zaidi na mikopo ya elimu ya juu kati ya mwaka 2022 hadi 2025 miongoni mwao kwa mwaka 2024/2025 wanawake wakiwa 5,000 (sawa na asilimia 48) na wanaume 5,464 (sawa na asilimia 52 ) ukilinganisha kwa mwaka 2021/2022 wanawake wakiwa 3,170 sawa (asilimia 43) na wanaume 4,175 sawa na (asilimia 57) .

Kuongezeka kwa idadi ya wanufaika wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kumechochea vijana wengi kujiunga na Elimu ya Juu na kuongeza udahili kwa Chuo kikuu Mzumbe ikiwa ni pamoja na wale wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini na hivyo kukifanya Chuo hiki kuwa miongoni mwa Taasisi muhimu zinazozalisha wataalamu wa ngazi mbalimbali wenye ujuzi na maarifa kwa ajili ya kujenga uchumi wa nchi yetu.

**Kuongezeka kwa ajira, kupanda madaraja na kulipwa malimbikizo ya watumishi wa**